# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

SIMU NA: 027 – 2552000
MOB NA: 0677 - 010213
FAX NA: 027 - 2552020
Email: ded@kitetodc.go.tz
info@kitetodc.go.tz

OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P. 98,
**KIBAYA - KITETO**

**Kumb. Na. HMW/KT/V/21/VOL.I/101** **10 Septemba, 2020**

## YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:**

### MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 1)

**SIFA ZA MWOMBAJI:**
Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) na cheti cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi

**KAZI NA MAJUKUMU:**
(i) Kutafuta kumbukumbu / nyaraka/ majalada yanayohitajika na wasomaji
(ii) Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu wa nyaraka.
(iii) Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/ nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
(iv) Kuweka/ kupanga kumbukumbu / nyaraka katika reki, katika Masjala vymba vya kuhifadhia kumbukumbu.
(v) Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka) kwenye majalada.

**MSHAHARA:**
Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi.

**MAELEZO YA JUMLA NA UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:**
1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe na nakala za vyeti vya elimu, taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha ndogo mbili za rangi (passport size).
3. Waombaji wote waaambatanishe na maelezo binafsi yaliyojitosheleza na yawe na anuani na namba ya simu.
4. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
5. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (Original Certificates).
6. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto,**
**S.L.P 98,**
**KIBAYA – KITETO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **27/09/2018** saa **9:30 Alasiri.**

Tamim H. Kambona
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KITETO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KITETO